JINA: ……. NAMBARI YAKO: …….

SHULE: ……..… DARASA…….……..

SAHIHI……. TAREHE: ……

102/3
KISWAHILI
Kidato cha nne
Karatasi ya Tatu
Machi 2013
Muda: Saa 2½

CROSS COUNTRY JOINT REGISRATION EXAM – 2013

Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)

KISWAHILI
Karatasi ya Tatu
Saa 2½

MAAGIZO

- Jibu maswali **manne** pekee. Swali la kwanza ni la **lazima**.
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki:
  Yaani: Ushairi, *Riwaya na Hadithi Fupi*, *Tamthilia*.
- Usijibu maswali **mawili** kutoka katika **sehemu moja**.
- Kila swali lina alama **20**.

A **SWALI LA LAZIMA**.

1. (a) Ngano ni nini? (alama 2)
   (b) Eleza tofauti iliyoko kati ya Hekaya na Hirafa. (alama 2)
   (c) Fafanua sifa zozote za ngano. (alama 6)
   (d) Fafanua umuhimu wa Fasihi Simulizi katika jamii. (alama 10)

B **USHAIRI**

Jibu swali la **pili** au la **tatu**.

2. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali*:

Hakika siku ya leo, ni siku ya majivuno
Basi pasiwe na choyo, na **usonono**
Tulekezane yaliyo, unawiri Muungano.

Tuzisafisheni nyoyo. Pasiwe na miguguno
Yaongoke tutakayo, kusiwe na mabishano
Mbegu hii tupandayo, ilete mema mavuno.

Tufuugulie upeo, Mola usiye mfano
Pa kitasa na komeo, tupite bila kinzano
Tupitishe njia hiyo, pasina masongamano

Twakuomba uumbao, mkono **vyanda** vitano
Tushikane hii leo, tuwe moja tangamano
Tupendane kwa pumbao, hali na maridhiano

Aliye ana machukiyo, adui wa Muungano
Naazibe masikiyo, asisikie maneno
Kisha awe kibogoyo, asiwe na moja jino.

Ya Ilahi ujalie, huu wetu Muungano
Nuru yake izagae, na nguvu za mapigano
Hasidi mpe hakie, mateso yaso mfano

Watamati komeleo, kuimba kwangu hukuno
Nataka maendeleo, yasiyo na malumbano
Daima tuwe ni ngao, palipo **msagurano**.

Maswali:
(a) Toa kichwa cha shairi hili. (alama 2)
(b) Shairi hili ni la bahari gani? Taja **mbili** (alama 2)
(c) Taja sifa tano za kiarudhi katika shairi hili. (alama 5)
(d) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. (alama 3)
(e) Eleza maana ya mshororo ufuatao: Pa kitasa na komeo, tupite bila kinzano. (alama 3)
(f) Huku ukitoa mifano **mitatu** eleza uhuru wa ushairi katika shairi hili. (alama 3)
(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (alama 3)
   (i) Usonono.
   (ii) Vyanda
   (iii) Msagurano.

AU

3. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali*:

Fani ya penzi kubwa, haishi kwa kuandika,
Yaliyompata Ubwa, kwa hivi hapa nataka,
Kujulishwa na Bi. Ubwa, apate kuelimika,
Lenye maana **huzibwa**, kama halikuandikwa,
Ama pengine huibwa, na moyo likatoka,
Sahau mwizi mkubwa, wa yote ya kukumbuka.

Unapotazama hasa, ushawishi wa mapenzi,
Kulinganisha anasa, zenye thamani azizi,
Bila ya kupapasa, huonyesha waziwazi,
Kuwa kale hata sasa, mapenzi yana enzi,
Hiyo bora kabisa, kwa kuunga jozi jozi,
Viumbe bila makosa, kila mmoja kwa mwenzi.

Yana nguvu halisi, kwa mtu yanapofika,
Hupenya moyo upesi, hayaachi yakishika,
Na shabaha hayakosi, yanapolenga hufika,
Hupunguza wasiwasi, ama hukuza mashaka,
Huweza na **hufilisi**, ama kuleta baraka,
Hasa katika nafsi, ambazo zinayataka.

Ajabu yanavyounga, duniani walimwengu,
Urafiki wakajenga, wale tamu na uchungu,
Bila ya kujitenga, kama ardhi na mbingu,
Moyoni yanapotunga, nguvu zake kama pingu,
Moyo yanapoufunga, macho huwa na ukungu,
Mtu akawa mjinga, bali ndiyo ulimwengu.

Mapenzi yakihimili, mfanowe sawasawa,
Kama mti wa kivuli, pumziko la kukaa,
Hushawishi kwa halali, roho kukaa **bia**,
Hustawisha na mwili, furaha moyo kutia,
Huweza na kubadili, wagombao zao mia,
Yana kumbuko ghali, mapenzi yasiyo **ria**.

Mapenzi hulinganika, na chumvi ya maisha,
Wakati yakikushika, haja njema yanapokanusha,
Utaona umewaka, moyo ndani na kuwasha,
Penzi kwa mali haraka, tabu mwangu likibisha,
Kwa dirishani hutoka, mvi likakuotesha.

Maswali

(a) Hili ni shairi la aina gani? (alama 2)
(b) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (alama 3)
(c) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 5)
(d) Fafanua ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa sita. (alama 2)

(e) Kwa mujibu wa shairi hili, mapenzi yanaweza kuleta hasara.
Toa mifano minne ya hasara hizo katika shairi. (alama 4)

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo: (alama 4)
(i) huzibwa
(ii) hufilisi
(iii) bia
(iv) ria

C RIWAYA: *Utengano – S.A. Mohamed*

Jibu swali la **4** au la **5**

4. "Mui huwa mwema". Thibitisha kauli hii kwa kuerejelea wahusika wanne. (alama 20)

5. "Wacha nikueleze kadhia yangu. Yako utaona si chochote."
(a) Weka dondoo hii katika muktadha wake. (alama 4)
(b) Fafanua kadhia aliyodokeza mnenaji wa maneno haya. (alama 8)
(c) Taja na ueleze sifa zozote mbili za mnenaji. (alama 4)
(d) Anayezungumziwa ana umuhimu upi katika kukuza maudhui ya mwandishi? (alama 4)

D TAMTHILIA: *Mstahiki Meya – T.M. Arege*

6. "Hali ya uongozi wa mji wa Cheneo na matatizo ya raia wake ni sawa na iliyo katika nchi za ulimwengu wa tatu." Thibitisha ukweli wa kauli hii. (alama 20)

E HADITHI FUPI: *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine – Ken Walibora na S.A. Mohamed*

7. (a) <u>Samaki wa nchi za joto</u>
"Wewe baradhuli, kwa nini hukusema jambo lolote. Maana?"
(i) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
(ii) Taja na ueleze tamathali ya usemi iliyotumika hapa. (alama 2)
(iii) Taja na ueleze sifa zozote tatu za msemaji wa maneno haya. (alama 6)

(b) Onyesha jinsi ambavyo maudhui ya ubaguzi yalivyosawiriwa katika hadithi *Damu Nyeusi*. (alama 8)